TANGAZO LA SERIKALI NA. 1005 la tarehe 20/11/2020

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

SURA 290

# SHERIA NDOGO

*(Imetungwa chini ya Kifungu cha 7(1) na 16 (1)*

## SHERIA NDOGO ZA ADA NA USHURU ZA HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA ZA MWAKA 2020

Jina

**1**. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima za Mwaka 2020.

Matumizi

**2**. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Itilima.

Tafsiri

**3**. Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya huduma, vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi wa umma yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia Sheria Ndogo hizi;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Itilima;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Mkurugenzi kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima au Afisa yeyote

aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa na Halmashauri kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hizi.

Utozaji wa ada na ushuru

4.- (1) Halmashauri itatoza ada na ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ada zinazotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi zitalipwa kwa Halmashauri.

(3) Kwa kuzingatia masharti ya kifungu kidogo cha (1), ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kwa Halmashauri au Wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(4) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hizi.

(5) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (4), Halmashauri inaweza kukubaliana na walipa ushuru wakubwa kuweka utaratibu maalum wa kulipa ushuru.

Wajibu wa kulipa ada na ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hizi.

Muda wa kukusanya ada na ushuru

6.- (1) Muda wa kukusanya ada na ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda uliotajwa hapo juu.

(4) Malipo ya ada na ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au Wakala wake na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama uthibitisho wa malipo yaliyofanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

7.- (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au Wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru kwa mujibu wa masharti ya Sheria Ndogo hizi.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru unaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zisizoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama, itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ada au ushuru unaodaiwa, gharama za kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata.mali au bidhaa bila kupata idhini ya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

bidhaa au mali iliyokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo umesababishwa na Halmashauri au Wakala.

Uteuzi wa Wakala

8.- (1) Halmashauri inaweza kuteua kampuni iliyosajiliwa kwa mujibu wa sheria kukusanya ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kukusanya na kupokea ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoidhinishwa katika Sheria Ndogo hizi;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9. Bila kuathiri masharti yaliyowekwa na Sheria Ndogo hizi, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi.

Makosa na adhabu

10.- (1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi na akipatikana na hatia atahukumiwa adhabu isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani kifungo na faini.

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

(c) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu huduma zinazohitaji kibali au leseni ya Halmashauri au shughuli zinazohitaji kulipiwa ushuru.

(2) Mtu yeyote atakayetiwa hatiani kwa kukiuka masharti ya kifungu kidogo cha (1) (b) na (c) atahukumiwa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini au kifungo kisichopungua miezi sita au vyote kwa pamoja kifungo na faini.

Kufililisha kosa

11. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufililisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi kiasi cha shilingi elfu thelathini endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

# JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa Chini ya kifungu cha 4(1))*

## Sehemu ya I:
## Ushuru wa Mazao

| Na | Aina ya Mazao | ushuru na kipimo |
|---|---|---|
| 1 | Pamba | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa tani moja |
| 2 | Nafaka mazao ya biashara | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa tani moja |
| 3 | Samaki na mazao ya samaki | 2% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo moja |
| 5 | Dagaa | 2% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo moja |
| 6 | Mazao ya mikunde | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa tani moja |
| 7 | Nafaka- Mazao ya Chakula | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa tani moja |
| 8. | Unera/mkonge | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa tani moja |
| 9. | Ushuru wa mashudu ya pamba/alizeti/mpunga | 3% ya bei ya mauzo sokoni kwa kilo moja |

## Sehemu ya II:
## Ada ya Ukaguzi wa Nyama

| Na | Aina ya mifugo | Ada |
|---|---|---|
| 1 | Ng’ombe | Tsh 1,500/= |
| 2 | Mbuzi | Tsh 800/= |
| 3 | Kondoo | Tsh 800/= |
| 4 | Nguruwe | Tsh 800/= |
| 5 | Kuwamba na kukausha ngozi<br>i. N’gombe/ Punda | Tsh 200/= |
| | ii. Mbuzi/kondoo | kwa 100/= |
| 6 | Kuogesha wanyama (josho) | @ Tsh 200/= |
| 7 | Kibali cha machinjio | Tsh 30,000/= kwa mwaka |
| 8 | Ada ya kusafirisha ngozi | Tsh 500/= kwa mfugo |
| 9 | Ada ya chapa ya mifugo | @ Tsh 500/= |

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

Sehemu ya III:
Ushuru wa Kushusha Mizigo katika Eneo au Soko lolote lililotengwa na Halmashauri

| Na | Aina ya chombo cha usafirishaji | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1 | uzito wa kuanzia tani 1 – 5 | Tsh 2,000/= |
| 2 | uzito wa kuanzia tani 6 – 10 | Tsh 5,000/= |
| 3 | uzito wa kuanzia tani 11 – 20 | Tsh 10,000/= |
| 4 | uzito wa kuanzia tani 20 – 50 | Tsh 20,000/= |

Sehemu ya IV:
Ushuru wa tandiko, meza au kizimba kwa mfanyabiashara asiyekuwa na Kitambulisho cha Ujasiriamali

| Na | Bidhaa | Kiasi cha ushuru |
|---|---|---|
| 1 | Tandiko 1 | Tsh. 500/= kwa siku |
| 2 | Kuku | Tsh. 1,500/= kwa tenga |

Sehemu ya V:

Ada ya Kibali

| Na. | Aina ya kibali | Ada ya Kibali (Tshs). |
|---|---|---|
| 1. | Tamasha | Tshs 50,000/= kwa siku |
| 2. | Michezo | Tshs 10,000 /=kwa siku |
| 3. | Mbio za Baiskeli | Tshs 20,000/= kwa mchezo |
| 4. | Mechi za mpira | 1 Tshs 0,000/= kwa ligi |
| 5. | Kuchezesha disko, maonesho ya bendi, Harusi, Matambiko, jando na unyago, sanaa za maonesho | Tshs 20,000/= kwa kibali |
| 6. | Upekuzi wa Jalada (Official search) | Tshs 40,000 kwa tukio |
| 7. | Bahati nasibu ndogondogo | Tshs 50,000/= kwa mchezo |
| 8. | Ngoma za utamaduni zenye kuingiza faida kifedha | Tshs 5,000 |
| 9. | Maonesho ( exhibition) ya ndani ya nchi | Tshs 5,000 banda kwa siku |
| 10 | Maonesho ( exhibition) ya kimataifa | Tshs 500,000 tukio zima. |

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

Sehemu ya VI:
Ada ya zabuni

| Na | Aina ya Zabuni | Kiwango cha Ada (Tshs) |
|---|---|---|
| 1. | Zabuni ya ujenzi wa majengo, barabara na miundo mbini mingine | Tsh. 100,000/= |
| 2. | Zabuni za uwakala mbalimbali | Tsh. 50,000/= |
| 3. | Zabuni za ugavi wa huduma | Tsh 70,000/= |

Sehemu ya VII:
Ada ya kukodi Mali za Halmashauri

| Na. | Vifaaa | Ada |
|---|---|---|
| 1 | Mitambo ya Halmashauri | Tsh 100,000/= kwa saa |
| 2 | Lori tani 7 hadi 10 bila mafuta | Tshs 3,000/= kwa kilometa |
| 3 | Gari ndogo lolote bila mafuta | Tshs 100,000/= kwa siku |
| 4 | Ukumbi wa Mkutano wa Halmashauri:<br>i. Ukumbi mdogo<br>ii. Ukumbi mkubwa | <br>Tshs 150,000/= kwa siku<br>Tshs. 350,000/= kwa siku |
| 5 | Kiti au meza za ukumbi wa mkutano wa Halmashauri | Tshs 500/=@ kiti 1 kwa siku<br>Tsh 1000/=@ meza 1 kwa siku |
| 6 | Maeneo ya wazi/ barabara kwa ajili ya shughuli za promosheni na matangazo ya biashara | Tshs 20,000/= kwa siku |
| 7 | Mashamba ya Halmashauri | Tshs 50,000/= kwa ekari kwa msimu |
| 8. | Kukodisha Trekta. | Kulingana na bei ya soko ya ekari |
| 9. | Mali nyingine ambayo haikutajwa | Kiwango kisichopungua 40,000 na kisichozidi 500,000 |

Sehemu ya VII:
Ushuru wa stendi na maegesho katika maeneo ya umma

| Na | AINA YA GARI | USHURU | IDADI |
|---|---|---|---|
| 1 | Mabasi /malori | Tsh, 3,000/= | Kwa siku |
| 2 | Kosta/Hiace | Tsh, 2,000/= | Kwa siku |

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Taxi | Tsh 1,000/= | Kwa siku |
| 4 | Bajaji | Tsh,1,000/= | Kwa siku |
| 5 | Magari ya watu binafsi | Tsh. 500.- | Kwa saa moja |

Sehemu ya VIII:
Ushuru wa Madini ya Ujenzi

| S/NO | AINA YA MADINI | USHURU UJAZO |
|---|---|---|
| 1 | Changarawe/mchanga/kokoto/mawe/kifusi inayobebwa kwa bajaji na mikokoteni | Tsh. 2,000/= kwa tripu |
| 2 | Changarawe /mchanga/ kokoto /mawe/ kifusi inayobebwa kwa gari | Tsh. 5,000 kwa tripu ya mita za ujazo $2m^3$ - $3.5m^3$ |
| 3 | Changarawe /mchanga/ kokoto /mawe/ kifusi inayobebwa kwa gari | Tsh. 10,000 kwa tripu ya mita za ujazo $3.6m^3$ - $5.5m^3$ |
| 4 | Changarawe /mchanga/ kokoto /mawe/ kifusi inayobebwa kwa gari | Tsh. 15,000 kwa tripu ya mita za ujazo $5.6m^3$ - $7.5m^3$ |
| 5 | Changarawe /mchanga/ kokoto /mawe/ kifusi inayobebwa kwa gari | Tsh. 20,000 kwa tripu ya mita za ujazo $7.6m^3$ - $15.5m^3$ |

Sehemu ya IX:
Kodi ya pango na majengo mengine ya Halmashauri.

| Na | Aina ya Jengo | Kodi ya Pango | Muda |
|---|---|---|---|
| 1 | Vibanda ndani ya Soko | Tsh.30,000/= | Kwa mwezi |
| | Vibanda nje ya Soko | Tsh.50,000/= | Kwa mwezi |
| 3 | Vibanda ndani ya stendi | Tsh. 30,000/= | Kwa mwezi |
| 4 | Vibanda nje ya stendi | Tsh.50,000/= | Kwa mwezi |
| 5 | Nyumba ya makazi ya Halmashauri | Tsh.20,000 mpaka 30,000/= | Kwa kila mpangaji kwa mwezi. |

Sehemu ya X:
Ada za huduma za Ardhi

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1 | Upimaji wa shamba | Tshs 10,000/= | Ekari moja |
| 2 | Ada ya survey | Tshs 20,000/= | Kwa ekari moja |

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3 | Kuoneshwa mipaka | Tshs 30,000/= | Kwa kiwanja kimoja |
| 4 | Kurudisha Kigingi | Tshs 50,000/= | Kwa kiwanja kimoja |

## JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya kifungu cha 11)*

### FOMU YA KUKIRI NA KUFILILISHA KOSA

Mimi ……………………..…...................… mwenye Namba ya Simu ………………………………….ninakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………..........……. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima kwamba mnamo tarehe …..… ya mwezi …..…. mwaka …........… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …… cha Sheria Ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Itilima za Mwaka 2020. Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi, niko tayari kulipa kiasi cha shilingi elfu thelathini na kutimiza wajibu wangu chini ya Sheria Ndogo hiyo badala ya kushtakiwa Mahakamai.

leo tarehe…………………………ya
Mwezi……………………Mwaka…………

Mbele ya;
Jina…………………………cheo……………………….
Saini…………………………………….
Tarehe…………………………………..

*GN. NO. 1005(Linaendelea)*

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya ya Itilima imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Halmashauri ya Wilaya ya Itilima uliofonyika tarehe 08-09 mwezi Mei mwaka 2019 mbele ya:-

………………………………

Elizabeth M. Gumbo

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA**

………………………………

Mh. Daudi M. Nyalamu

**MWENYEKITI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA ITILIMA**

**NAKUBALI**

……………………………….

Mhe. Selemani S. Jafo (Mb),

**WAZIRI WA NCHI – OR –TAMISEMI**

Dodoma

Tarehe 28 Septemba, 2020